
# DIWANI KAMA

# WAKALA WA MAMLAKA



## Kitabu 10

MAFUNZO KWA VIONGOZI WALIOCHAGULIWA
ISTANBUL, 1996 – MKUTANO MKUU WA JIJI

ISBN kwa seti kamili vitabu 13: 92-131242-6
ISBN kwa kitabu hiki: 92-1-131253-1
HS/334/94 Swahili version

# DIBAJI

Kama ambavyo imeonyeshwa na ukaguzi wa mahitaji ya mafunzo uliofanywa na Kituo cha Umoja wa Mataifa cha Makao ya Binadamu (Habitat), mahitaji ya mafunzo ya maofisa wa serikali ambao wamechaguliwa (madiwani) au ya wanasiasa, yanaonekana ya dharura sana kote ulimwenguni. Wakati huo huo, mafunzo haya yanaonekana katika maeneo yenye kushugulikiwa kwa kiwango cha chini zaidi miongoni mwa yale yanayo jenga uwezo kwa minajili ya maendeleo ya mneneo maalum na usimamizi wa miji.

Kwa miaka michache iliyopita, nchi zinazotofautiana sana kama vile Nepal na Poland au Uganda na Paraguy zimeanza, kwa mara ya kwanza kwa muda wa miongo mingi, na wakati mwingine kwa mara ya kwanza kabisa, utaratibu wa kuchagua madiwani na mameya. Mahitaji ya mafunzo ya maofisa waliochaguliwa wa serikali za mitaa yanapewa umuhimu mkubwa katika miji yenye demokrasia iliyoimarika kama vile Ecuador, India na Marekani.

Ili kushughulikia mahitaji haya, kituo cha Umoja wa mataifa cha Makao ya Binadamu (Habitat), kimetayarisha na kufanyia majaribio mfululizo wa vitabu vya kufunzia ili kusaidia madiwani kuwawakilisha wananchi, kutoa uongozi wa kiraia, na kwa njia ya kufaulu kufanya kazi na serikali kuu na pia wafanyikazi wa kiusimamizi na kitaaluma katika serikali za mitaa na taasisi nyingine za serikali za mitaa. Vitabu hivi vinahusu sera na uundaji mipango, mawasiliano, kuhawilisha na uongozi, kuhudhuria, kusimamia na kuendesha mikutano, shughuli za madiwani za kuwaongezea uwezo, usimamizi wa pesa na mahitaji mengine yanayokaribiana na hayo.

Kitabu hiki, *Diwani kama wakala wa mamlaka,* ni kimojawapo cha mfululizo wa vitabu 12 na kimenuiwa kutumiwa hasa na wakufunzi katika taasisi za mafunzo za kitaifa zinazohudumia serikali za mitaa au sehemu za masomo za serikali za mitaa zenyewe. Kama usaidizi zaidi kwa wakufunzi wakitumia vitabu hivi, Kituo cha Umoja wa Mataifa cha Makao ya Binadamu (Habitat) kimechapisha kitabu cha kuandamana na vitabu hivyo, kiitwacho *Mwongozo kwa Wakufunzi wa Masomo kwa Viongozi Waliochaguliwa* kilicho na maelezo na habari kwa mkufunzi, kilichotayarishwa kwa manufaa ya wakufunzi hawa katika kupanga warsha za viongozi waliochaguliwa kwenye serikali za mitaa, kwa kuzingatia vitabu hivi.

Inatarajiwa kwamba kitabu hiki kitachangia kwa kiwango kikubwa uimarishaji wa uwezo wa serikali za mitaa kupitia kutumiwa kwa taratibu nzuri za uongozi - mojawapo ya malengo makuu ya Kongamano la Umoja wa Mataifa juu ya Makao ya Binadamu, Habitat II.

Ningependa kuwashukuru Dkt. Fred Fisher na Bw. David W. Tees kwa sababu ya kutayarisha kitabu hiki na vitabu vingine katika mfululizo huu wakishirikiana na wafanyikazi wa Kituo cha Umoja wa Mataifa cha Makao ya Binadamu (Habitat), Sehemu ya Masomo katika miradi ya masomo ya Kituo inayothaminiwa na Serikali ya Uholanzi. Pia ningependa kutaja mchango wa wakufunzi na maofisa wa serikali za mitaa wa Costa Rica, El Salvador, Kenya, Lithuania, Romania na Uganda ambao walisaidia kufanyia majaribio mfululizo wa vitabu hivi vya kufundishia.

Dkt. Wally N'Dow
Naibu wa Katibu – Mkuu
Kituo cha Umoja wa Mataifa cha Makao ya Binadamu (Habitat)

## *KUHUSU KOFIA*

Kofia ambayo imevaliwa na mtu aliye upande wa kulia na ambayo imeonyeshwa kwenye kurasa zinazofuata ilichaguliwa kuwakilisha jukumu la diwani linaloshughulikiwa katika kitabu hiki.



Kofia ya ufumwele inayovaliwa na waendeshaji ngamia wa Yemen.

# UTAKAKOKIPATA KATIKA KITABU HIKI


| | Ukurasa |
|---|---|
| Namna ya kutumia kitabu hiki | 4 |
| **Sehemu I** | 4 |
| Insha juu ya diwani kama wakala wa mamlaka | 4 |
| Maelezo | 4 |
| Muhtasari | 4 |
| Tafakari | 5 |
| Dhana na Mawazo | 5 |
| Mtu mmoja au kundi? | 6 |
| Tafakari | 7 |
| Mawazo mbali mbali juu ya mamlaka | 8 |
| Wewe na waajiriwa wako | 9 |
| Kujenga ushirikiano mwema | 10 |
| Mambo muhimu | 10 |
| Marejeleo | 11 |
| **Sehemu II** | 11 |
| Warsha juu ya diwani kama wakala wa mamlaka | 11 |
| Mtazamo wa kijumla | 11 |
| 10.1 Zoezi la kuamsha mwili na akili: Baraza la mji lenye mamlaka makubwa | 12 |
| 10.2 Zoezi: kutayarisha ramani ya mahusiano ya mamlaka | 12 |
| 10.3 Wasilisho la mkufunzi | 14 |
| 10.4 Kujitathmini: hojaji juu ya kujipa mamlaka | 14 |
| 10.5 Zoezi: visa muhimu sana katika utumiaji wa mamlaka | 16 |
| 10.6 Zoezi la kusihili ujuzi | 18 |

# NAMNA YA KUTUMIA KITABU HIKI

Kama vitabu vingine katika mfululizo huu, kitabu hiki cha mafunzo juu ya *WAKALA WA MAMLAKA*, kinaweza kutumiwa kwa njia mbali mbali.

### *Kujifunza mtu binafsi*

Insha inayofungua kitabu hiki imenuiwa kutumiwa katika kujifunza mtu binafsi. Unachohitaji ni mahali palipo kimya ili kufikiria, wakati, na kitu cha kuandikia. Ili kupata matokeo mazuri kabisa, tunakuhimiza kuandika majibu ya maswali yanayoulizwa mara kwa mara katika insha. Manufaa ya kimasomo kutoka habari zilizomo humu yanaongezeka mara kadha kwa msomaji anayezingatia jambo hili.

### *Mafunzo kwa warsha*

Hati za mkufunzi na mazoezi yaliyomo katika kitabu hiki yamenuiwa kutumiwa na wakufunzi wenye ujuzi katika warsha ya madiwani kutoka serikali za mitaa. Tumeweka humu shughuli za masomo na miundo mbali mbali ili kuwapa wakufunzi uwezo mkubwa wa kuifanya warsha kuwiana na mahitaji maalum ya madiwani wanaoshiriki. Imekuwa dhamira yetu katika kutayarisha kitabu hiki kukuhimiza kushirikisha tajriba yako kama mkufunzi ili kuimarisha ubora wa masomo ya mafunzo haya ya madiwani wanaoshiriki katika warsha.

Kama mkufunzi unaweza kuamua kutumia mambo yaliyomo humu katika mfuatilio na hali kama ilivyotolewa kwenye kitabu. Lakini ukipenda, unaweza kubadilisha mfuatilio au hali ya mambo haya kama inavyohitajika ili kutimiza shabaha kwenye hali maalum ya mafunzo. Unaweza kuamua kutoa mafunzo ya saa tatu, kwa kutumia mazoezi na shughuli za kimsingi zilizomo katika kitabu. Au unaweza kutumia mambo kadha yaliyomo katika kitabu huku ukiongezea habari zako ili kurefusha mafunzo hadi siku nzima.

Kitabu hiki ni kimojawapo katika mfululizo wa vitabu 12 vya kufunza viongozi waliochaguliwa. Unaweza kuamua au ukaombwa kutoa warsha inayokuhitaji kutumia zaidi ya kitabu kimoja au vitabu vyote kwa muda mrefu. Ingawa kila kitabu kinaweza kutumiwa peke yake, kutumiwa kwa vitabu hivi katika mfuatilio kunaweza kutoa tajriba imara na inayounga pamoja mambo mengi kwa madiwani wanaoshiriki katika warsha.

### *Kufunza kundi*

Vitabu hivi pia vinaweza kutumiwa bora zaidi kukiwepo na usaidizi wa mkufunzi mwenye tajriba ili kuboresha utendaji wa madiwani wanaohudumia katika kikundi kimoja cha utawala. Madiwani wanaohudumu pamoja wanapo-funzwa, mwelekezi wa mafunzo hana budi kuwa tayari kupanga shughuli za masomo zilizomo katika kitabu hiki kwa namna tofauti. Wakati mwingine wewe kama mwelekezi, waweza kuamua kuongeza shughuli mpya kulingana na hali na tabia za kundi linalohusika. Tunatarajia katika hali kama hii,utachukulia kitabu hiki kama "sanduku la vifaa" lililo na mibadala mingi ya mawazo ya kufundishia ambayo yatachanganywa na kuwianishwa, kubadilishwa au kutupilowa mbali kama hali inavyohitaji.

Katika vitabu hivi kuna mibadala mingi ya kuchagua. Tunatumaini utanufaishwa navyo.

# SEHEMU I

# INSHA

# DIWANI KAMA WAKALA WA MAMLAKA

### *Maelezo*

Diwani, katika jukumu la WAKALA WA MAMLAKA, hutumia uwezo wake wa kibinafsi na vile vile mamlaka ya cheo chake rasmi, ili kuwezesha mambo kufanyika.

### *Muhtasari*

Insha hii inahusu mada ngumu ya mamlaka kama yanavyohusiana na kazi yako kama kiongozi aliyechaguliwa. Tutapitia baadhi ya maelezo ya jadi ya mamlaka na kuchunguza njia ambazo viongozi waliochaguliwa wanaweza kutumia ili kufaulu zaidi kama wakala wa mamlaka. Pia tutazungumzia ukweli kwamba hili ndilo jukumu lenye uwezekano mkubwa wa kutumiwa vibaya.

### *Tafakari*

Ninapojifikiria kama wakala wa mamlaka, mambo yafuatayo hunijia akilini:

1. ____________________________________________________________

2. ____________________________________________________________

3. ____________________________________________________________

### *Dhana na mawazo*

Maelezo tuliyojipa jukumu lako kama wakala wa mamlaka yanakinzana na ugumu wake. Mwanasayansi mmoja wa kisiasa alifananisha mamlaka na "mojawapo ya zile dhana za kutisha za hema kubwa ambamo sarakasi ya angalau duara tatu inaendelea". Max Weber, mwanasosiolojia wa Kijerumani, ambaye ni maarufu kutokana na maelezo yake juu ya urasini, aliwahi kusema:

> *Mamlaka ni uwezekano kwamba mshiriki mmoja katika mahusiano katika jamii atakuwa na uwezo wa kufanya yale atakayo, licha ya pingamizi, bila kutilia maanani msingi wa uwezekano huu*[(1)]

Tunaweza kwenda mbali tukijaribu kuelezea mamlaka lakini hatuna hakika kwamba jambo hilo lina manufaa.

Baadhi ya watu hata wanaweza kushuku hekima ya kushughulikia suala hili katika vitabu vya mafunzo kama hivi. Kuna mwenendo wa kuangalia mamlaka kwa njia zifuatazo:

"Mada ni ya kisiasa mno."

"Wanasiasa wa eneo hili wana mamlaka makubwa sana hivi sasakuliko jinsi wanavyoweza kuyatumia vizuri."

"Mamlaka ni jambo ovu, ambalo labda linahitajika, lakini hata ni jambo ovu, sidhani inafaa kulizungumzia."

"Madiwani hawahitaji mamlaka zaidi. Usiwape mawazo zaidi."

Kwa bahati mbaya, hoja kama hizi zina ukweli wa namna fulani. Hatutaenda mbali sana kabla ya kupata mifano ya utumiaji mbaya wa mamlaka miongoni mwa viongozi waliochaguliwa au kutumiwa vibaya kwa mamlaka ambayo yametolewa kwa ofisi. Tungekuwa hatufahamu mambo tungefikiria kwamba hakuna mtu agombeaye cheo cha umma kwa sababu ya "kutaka kutajirika", au kwa sababu "wana kisasi cha kisiasa cha kulipiza". Kutumiwa vibaya kwa mamlaka katika eneo dogo labda ndiyo matumizi mabaya zaidi ya mamlaka kwa sababu ni kitendo dhidi ya jirani. Katika kiwango cha taifa, sura za majirani zetu hazionekani vizuri na utumiaji mbaya wa mamlaka si wa mtu kwa mtu mwingine.

Sote tunajua kwamba unaweza kutumia vibaya cheo chako kama diwani. Lakini kuna upande mwingine wa jambo hili. Mamlaka unayochukuliwa kuwa nayo unapochukua madaraka ya ofisi yako kama kiongozi aliyechaguliwa pia ndio msingi mkubwa kabisa wa nguvu ambazo hazijapevuka bado unaweza kutumia ili mambo yatimizwe kwa manufaa ya jamii yako. Labda umegundua kwamba tulitumia neno "madaraka" katika jaribio la kuelezea msingi wa mamlaka yako. Baadhi ya watu wanaweza kutoa kauli kwamba mamlaka na madaraka sawa, lakini tunafikiria kwamba haya ni mambo mawili tofauti; tofauti kwa kiwango cha kutosha kutumia muda mfupi tukionyesha tofauti tunazofikiria zipo baina ya mambo haya.

Madaraka ni muundo wa kisheria ambamo wewe na madiwani wengine mnafanya kazi ili mambo yatekelezwe kwa niaba ya jamii yako. Madaraka ni mfumo unaowekwa ili kutekeleza maadili ya pamoja. Madaraka ni kibali kinachotolewa kwako na kwa baraza kihalali ili kuendesha mambo fulani na kutumia rasilmali ili kufikia malengo ya pamoja au ya jamii. Madaraka yako kama diwani, ndio msingi wako halali au rasmi wa mamlaka, lakini sio msingi wa pekee wa mamlaka unaoweza kutumia ili kutimiza mambo.

Mamlaka yamekuwa mada ya kusisimua akili kwa wanasiasa na wanaakademia kwa muda mrefu kwa kadri ambayo makundi haya yaliweza kufikiria mada hii. Na wanaakademia wamekuwa wakijaribu kuainisha misingi ya mamlaka kwa muda mrefu kwa kadri ambayo wanasiasa na watu wengine wamekuwa wakiwapima kuhusiana na jambo hili. French na Raven ni watu wawili ambao wamefaulu kufafanua misingi ya mamlaka. Ufafanuzi wao ni miongoni mwa fafanuzi ambazo zimefaulu sana. Aina wanazofafanua ni:

1. Mamlaka ya tuzo yana msingi kwenye imani yangu kwamba unaweza kutoa tuzo - kupandisha cheo, kufanyia hisani, kutambuliwa, kufikia rasilmali;

2. Mamlaka ya kushurutisha yanatokana na hisia yangu kwamba una uwezo wa kuadhibu - kutia uchungu, kuzomea, kuteremsha cheo na kuondoa hisani;

3. Mamlaka halali yana msingi kwenye cheo chako rasmi katika jamii. Cheo hiki kinakupa haki ya kutumia mamlaka kwangu na kwa watu wengine;

4. Mamlaka ya kujitambulisha yanatokana na kujitambulisha na mtu ambaye ana sifa za kibinafsi ambazo zinasababisha apewe heshima na utiivu;

5. Mamlaka ya kitaalam yanatokana na imani yangu kwamba unamiliki ujuzi maalum, stadi au utaalam; na

6. Mamlaka ya habari yana msingi kwenye imani yangu kwamba una habari, au njia za kufikia habari ambazo ni muhimu kwangu.(2)

Kwa aina sita za mamlaka zilizofafanuliwa na French na Raven, tunataka kuon-geza mbili zaidi ambazo tunaamini zinapatikana sana katika tajriba ya viongozi waliochaguliwa. Hizi ni:

7. Mamlaka ya mahusiano yana msingi kwenye imani yangu kwamba wewe, kama diwani, una uhusiano na watu wenye uwezo au muhimu; na

8. Mamlaka ya changamoto yanatokana na uwezo wako wa kuleta pamoja misingi miwili au zaidi ya mamlaka, kila mojawapo ya misingi hiyo ikiwa labda haina uwezo wa kuleta matokeo.

Hebu tuangalie kwa undani misingi hii inayoweza kutoa mamlaka. Misingi mitatu ya mwanzo (tuzo, kushurutisha na halali) inatokana na ofisi yako rasmi. Hii ni misingi inayoweza kutoa mamlaka inayokujia moja kwa moja kupitia kuchaguliwa kwako kama diwani. Pia inakupa uwezo wa kubadilisha tabia ya mtu mwingine hata anapokuwa anapinga juhudi zako. Na hayo ndiyo mamlaka hasa!

Unaweza tu kutumia misingi mingine inayofuata ya mamlaka (habari, kujitambulisha, utaalam na mahusiano) ikiwa watu wanaamini kwamba unayo misingi hiyo. Yaani, ikiwa unaamini kwamba wewe ni mtaalam katika eneo fulani la ujuzi wa juu lakini hakuna mtu mwingine anayefikiria hivyo, huo si msingi wa mamlaka unaoweza kutumia. Unaweza kubadilisha hali hiyo, ikiwa utawashawishi watu kwamba wewe kweli ni mtaalam. Jambo hili ni kweli pia kwa misingi mingine. Kwa mfano, inawezekana kuwa ni kweli kwamba una "mahusiano" lakini mahusiano hayo hayawi msingi wa mamlaka ikiwa wale ulio na mahusiano nao hawaonyeshi hivyo kwa vitendo. Yaani, misingi hii ya mamlaka inahitaji vitendo vya pande mbili-vyako na vya watu wengine-kabla ya kuwa mibadala ya kutoa uwezo ambao unaweza kutumia ili kutekeleza mambo.

Msingi wa mwisho wa mamlaka, mamlaka ya changamoto, hutegemea ubunifu wako katika kuona namna mseto wa misingi ya mamlaka unaweza kukupa uwezo wa kufanya yale unayotaka kufanya. Baada ya utambuzi huo, bila shaka unahitaji uwezo wa kuweka misingi hiyo pamoja kwa namna nzuri.

*Tandabui zinapoungana, zinaweza kufunga simba*

*- Methali kutoka Ethiopia*

### *Mtu mmoja au kundi?*

Namna nyingine ya kuangalia suala la mamlaka ni kama unaweza kufanya mambo peke yako au ikiwa unahitaji kutenda kwa ushirikiano na watu wengine. Tumezungumzia kipengele kimoja cha suala hili, kwenye msingi wa mamlaka yako ambayo umepewa na kanuni za ofisi yako. Ingawa mamlaka haya yamepewa kila diwani ni nadra kutumiwa na diwani mmoja mmoja. Si sharti hali iwe hivyo kwa meya au watu wengine ambao wanashikilia ofisi zenye mamlaka ambayo zimepewa kisheria. Lakini hebu tuangalie ile misingi ya mamlaka ambayo unapewa kama mtu mmoja katika kundi. Kwa jumla uwezo wako wa kutuza mtu au kundi au kuadhibu mtu au kundi (mamlaka ya kuadhibu) au kutumia kihalali msingi wa uwezo wako, haupo au umewekewa mipaka kwa kiwango kikubwa kwa kuwa wewe ni mtu mmoja tu katika kundi halali lenye mamlaka haya. Katika hali hii, msingi halisi wa mamlaka yako kwa wenzako haumo kwenye mamlaka ya aina za kutumia tuzo - shuruti - uhalali bali katika kutumia watu wengine. Ikiwa, kwa mfano, una sifa ambazo zinavutia kwa

madiwani wengine na kwamba hawako radhi kukubaliana nawe tu bali pia kupiga kura ili kukuunga mkono kwa sababu ya sifa hizi za kibinafsi, basi utakuwa umeongezea mamlaka yako.

Vivyo hivyo kwa utaalam. Ikiwa wenzako wanabaini kwamba unajua kuliko wao kuhususiana na jambo fulani linaloshughulikiwa, huenda wakakubaliana na maoni yako wanapofanya uamuzi kama kundi. Jambo hili litaongeza mamlaka yako ya kuwezesha mambo kutekelezwa. Lakini jambo hili halitokei kila mara. Sote tumeona hali ambapo mtu ana utaalam mwingi lakini hakuna anayetaka kumsikiza kwani hawavutiwi naye kwa sababu fulani au ameharibu sifa yake kama mtaalam kwa sababu moja au nyingine.

Misingi ya mamlaka inayotokana na habari na mahusiano ni migumu kuitathmini wakati watu wanapotenda kazi katika mfumo ambako mamlaka yamegawanywa kwenye kundi. Ukiwa na habari ambazo wengine hawana, na uzitumie vizuri na kwa wakati unaofaa, zinaweza kukupa mamlaka miongoni mwa wenzako wakati wa kupiga kura. Mmoja wa waandishi wa kitabu hiki alipata tajriba alipokuwa meneja wa jiji ambayo inathibitisha jambo hili. Jiji lilikuwa karibu kueneza mkataba mzuri sana wa utumiaji maji kwa kiwanda cha kusubia madini kilichotegemea vigezo ambavyo havikuwa na msingi, meneja wa jiji alipowaeleza wanabaraza kwamba kiwanda hicho kilikuwa kimetumia mali ya jiji kwa muda mrefu kwa namna ambayo haikuwa halali. (Baadhi ya mali hiyo ilihusisha mkataba huo mpya.) Habari hizi zilibadilisha kabisa uamuzi wa jiji kutoka ule wa kuunga kiwanda mkono hadi ule wa kukipinga. (Kufichuliwa kwa habari hizi karibu kusababisha meneja wa jiji kufutwa kazi. Iligundulika kwamba mwenye kiwanda alikuwa na "mamlaka ya uhusiano" na baraza kuliko meneja, wa jiji).

Mamlaka ya changamoto yana nguvu kuliko wengi miongoni mwetu tunavyotambua. Mara nyingi madaraka rasmi ya baraza hayatoshi kutekeleza miradi migumu au kuanzisha huduma zenye uwezekano wa kuleta mabishano au zenye ugumu. Katika hali hii labda ni bora kuchunguza hatua kwa hatua misingi ya mamlaka ambayo tumetambua ili kuamua kama kuna nafasi ya kutumia mchanganyiko wa misingi ya mamlama ili kufikia lengo lako.

Mamlaka ya mtu binafsi yanachukua sura tofauti ikiwa baraza limegawika kwenye vikundi viwili na diwani mmoja yumo katikati ya vikundi hivi. Huyu "mtu wa katikati" huenda asiwe na nguvu sana katika sifa zake za kibinafsi. Hata hivyo, watu katika hali hii wanaweza, kama inavyotokea mara nyingi, kuwa na uwezo ambao hawangekuwa nao katika hali ya kawaida. Tungependa kurejelea tajriba yetu ili kufafanua jambo hili.

Mmojawapo wa waandishi anaishi katika jumuiya ndogo ambamo baadhi ya wananchi walifanya mapinduzi ya kuchukua halmashauri ya elimu kwa sababu ya kupanda gharama na masuala mengine. ("Neno mapinduzi" linafanya jambo hili kuonekana la ajabu). Kwa hakika wananchi walifaulu kuwezesha watu watano kuchaguliwa kwenye uchaguzi wa mwisho mwisho. Kwa kuwa halmashauri ilikuwa na wanachama tisa walifaulu kupata watu wengi au mamlaka ya kuelekeza uamuzi na ajenda. Fanaka, ndio -lakini ya muda mfupi. Mmojawapo wa wanahalmashauri waliochaguliwa mwisho mwisho aliamua kwamba alipenda wanahalmashauri wa zamami na akavuka sakafu. Basi alifutilia mbali fanaka yote ambayo wenzake wa hapo nyuma na watu waliowaunga mkono walikuwa wamepata katika uchaguzi mkali wa kuchukua hatamu za mfumo wa shule. Hayo ndiyo mamlaka!

Kabla ya kuendelea, tunataka kukupa fursa ya kutafakari kwa muda mfupi kuhusu juhudi zako katika baraza au hali nyingine ambapo ulikuwa na nafasi ya kutumia mamlaka yako.

## *Tafakari*

Kumbuka mara moja au mbili hivi majuzi ambapo ulijihisi "una uwezo sana" kama diwani. Kulikuwa hali gani? Ni aina gani ya mamlaka unayofikiria ulikuwa ukitumia. Ni matokeo gani yaliyotokana na kutumia msingi huu wa mamlaka? Ikiwa ungepitia tajriba hii tena, ungefanya mambo kwa njia tofauti? Ikiwa ndio, kwa njia gani na kwa nini?

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

Sasa fikiria hali ambapo ulijihisi kwamba "hukuwa na mamlaka". Ilikuwa nini? Kwa nini ulihisi hivyo? Ni nani aliyekuwa na mamlaka katika hali hiyo? Unafikiria walikuwa wanatumia msingi gani wa mamlaka? Ungelikuwa na nafasi ya kupitia tajriba hiyo tena, ni jambo gani ambalo ungefanya kwa namna tofauti ili uwe na athari kubwa zaidi?

## *Mawazo mbali mbali juu ya mamlaka*

1. **Kwa nini viongozi waliochaguliwa wenye mamlaka rasmi makubwa wana matatizo katika kuwezesha mambo kufanyika?** Jambo hili linaharibu hali zaidi, au sivyo? Sababu mojawapo ni imani (au ni imani-uwongo?) kwamba mamlaka kwa kweli hutokana na ofisi au cheo cha udiwani. "Kanuni za Jiji zinasema kwamba ninaweza kufanya hili na lile. Lakini ninapofanya mambo haya hakuna jambo muhimu linalotendeka". Inawezekana kwamba wale ambao "hawamo kwenye mamlaka" (wasio na mamlaka) wanakataa kukubali maelezo yanayotolewa na wenye mamlaka juu yao wenyewe? Elizabeth Janeway, katika kitabu chake chenye kusisimua mawazo kiitwacho *Powers for the Weak*, anasema "utumiaji wa mamlaka uliopangika ili kutoamini ndiyo mamlaka ya kwanza ya wanyonge".[3] Na, kudhibiti mamlaka kwao kunaanza wanapokataa elezo kwamba walio mamlakani wamejiweka wenyewe.

   Karne nyingi zilizopita, katika Uyunani (Greece) Demosthenes alishauri watu wake kwamba:

   *Kuna ngao moja ya kawaida ya kujikinga katika hali ya mwerevu, ambayo ni usalama mzuri kwa wote. Ninamaanisha nini? Kutoamini upande mwin-gine. Weka jambo hili; lishikilie; lihifadhi jambo hili pekee, na huta-dhurika.*

   Labda ametia chumvi lakini anatoa mwangaza kuhusu utatanishi ambao viongozi wengi wa umma hukabiliana nao kunapokuwa na hali ya kutoaminiana. Wale ambao hawana uwezo wa kiuchumi na wa kijamii; na tunaweza kuongeza wale ambao wananyimwa haki za kisiasa, wana uwezo mkubwa wa kutoamini yale yanayotoka kwenye ofisi za serikali za mitaa kote duniani, hasa kuhusiana na sera. Huku kutoamini mara nyingi huwa kuna sababu na huwa ni mojawapo ya vikwazo vikubwa vinavyotatiza serikali ya mtaa.

2. Mamlaka yanachukuliwa kama jambo la kutoka juu kuelekea chini na la kutumiwa na wale wenye madaraka wakati ambapo katika uhalisi, mamlaka hutiririka kuelekea pande zote. Jambo hili linaweza kuaibisha watu wengi ambao wananuia kuingia kwenye "vyeo vya mamlaka". Baa-daye wanagundua kwamba kwa kiwango kikubwa mamlaka yao yamo kwenye uwezo wa wengine wa kuwaamini. Kwa diwani anayewakilisha jamii, ni jambo la kutia moyo kujua kwamba uwezekano wa kuipa jamii uwezo upo kila mahali.

预览已结束，完整报告链接和二维码如下：
https://www.yunbaogao.cn/report/index/report?reportId=5_19419